*ISSN* 3104-6371

# UTAMADUNI ZA HARUSI WA ZANZIBAR


| الناجح على سحيم الناجح | سالم محمود عبدالهادي مسعود | محمد يونس خليفه |
|---|---|---|
| Alnnajeh Ali Ashim | Salem Mahmoud Abdulhadi | Mohammed younis Khalifa |
| استاذ مشارك كلية اللغات | ماجستير .مساعد محاضر | استاذ مشارك كلية اللغات |
| Maji84242@gmail.com | lalnajh94@gmail.com | Mohammedyounis171@gmail.com |


**ARTICLE INFO**

***Received:*** 15-11-2025

***Accepted:*** 22-11-2025

***Published:*** 02-12-2025

**Ikisiri**

Utafiti huu utatoa taarifa kuhusu utamaduni wa harusi za Kizinzibari

Utafiti huu utatoa picha kamilin kuhusu harakati za harusi za Kiafrika

**Maneno Muhimu:** Harusi, Zanzibar , Utamaduni , Katika, Watu

**الملخص**

توفر هذه الدراسة معلومات حول تقاليد الزفاف في الزنجبار

وتقدم هذه الدراسة صورة شاملة لحركة الزفاف الأفريقية بشكل عام.

**الكلمات المفتاحية:** عرس، زنجيبار ، عادات، في، أشخاص

## SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1 USULI WA MADA

Harusi ni moja kati ya sherehe kubwa na adhimu kwa watu wa visiwa vya Unguja na Pemba. Siku hii hukutanisha watu wa aina mbali mbali kwa ajili ya kusaidia au kushuhudia tukio hili ambalo kwa kawaida hujaa furaha na bashasha kwa wahusika, wapenzi, marafiki, majirani na waalikwa. Kama ulivyo utamaduni wa kizanzibari ambao kwa sehemu kubwa umejengeka kwa mchanganyiko wa tabia za kiafrika na kigeni hususan kutoka bara la Asia (Arabu) na hata harusi za kizanzibari zimejengeka kwa tabia tofauti kama za kiafrika, kiarabu na hata kihindi.

Msingi wa pili mkuu wa harusi za kizanzibari ni imani zenye kuakisi jamii ya wazanzibi Imani hizi zimejikita katika sehemu mbili kuu uislamu na jadi. Imani mbili hizo ndizo zenye kuongoza na kuwa kama dira ya utekelezaji wa tukio zima kuanzia mwanzo hadi mwisho. Taswira hii huonekana katika kila nyanja za harusi ya kizanzibari kuanzia matendo, mavazi na hata mapambo yanayotumika.

### 1.2 TATIZO LA UTAFITI

Kwa kawaida harusi za kizanzibari hufanyika katika maeneo maalumu kama vile misikitini, vyuoni (madrasa), chini ya miti mikubwa iliyojirani na makaazi ya watu hasa vijijini. Miti mashuhuri sana inayotumika ni miembe. Makuti, miti, mikeka na majamvi hutumika kama ni vikalio kwa watu wote wanaohudhuria harusi hiyo. Bibi Mtumwa Haji Ame miaka 63 mkaazi wa kwa Boko mjini Zanzibar alieleza kwamba hapo zamani harusi za asili zilifanyika pia katika penu (baraza) kubwa ambazo hujengwa sehemu ya mbele ya nyumba ya mswahili.

Hata hivyo aliendelea kubainisha kwamba kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu jamii imeanza kutumia zaidi misikiti na madrasa na hii ni kutokana na imani na itikadi za wenyeji wa visiwa vya Zanzibar.

Kutokana na melezo ya watu mbali mbali waliohojiwa juu ya utamaduni wa harusi za kizanzibari wamebainisha kwamba harusi huwa na sehemu mbili kuu matayarisho (hatua za awali) na Akdi (Kufungisha Ndoa)

**1.3 Umuhimu wa Utafiti**

1. Utafiti huu utatoa taarifa kuhusu utamaduni wa harusi za Kizinzibari.
2. Utafiti huu utatoa picha kamilin kuhusu harakati za harusi za Kiafrika kwa jumla.
3. Utafiti huu utatoa picha kamilin kuhusu harakati za harusi za Kizinzibari hasa.
4. Utafiti huu utawasaidia watafiti wengine waendeleze zaidi katika kutafiti vipengele vingine vya utamaduni wa Aftika.

**1.4 Malengo ya Utafiti**

1. Kuchunguza sehemu ya matayarisho (hatua za awali) katika harusi za kizinzibari.
2. Kuchunguza sehemu ya Akdi (Kufungisha Ndoa) katika harusi za kizinzibari.
3. Kuonyesha kwa njia gani harusi za kizinzibari zinavyoendeshwa.

**SURA YA PILI**

**MATAYARISHO (HATUA ZA AWALI)**

**2.0 UTANGULIZI**

Sehemu hii ya harusi hujumuisha mambo mengi kama vile kuchagua mchumba, posa, singo/ unyago kupaka hina, kumfunza bi harusi na bwana harusi, na kupima nyumba kuangalia siku na mkesha wa harusi.

**2.1 Kuchagua Mchumba**

Kimila watoto wa kike na wakiume wa kizanzibari walichaguliwa wachumba na wazee wao baada ya kuonekana kuwa wameshakuwa tayari kuanza maisha yao ya kifamilia, hii huwa ni amri ya wazee na watoto hawapaswi kuhoji wala kwenda kinyume na amri hiyo. Mambo yanayoongoza utenzi wa wachumba ni undugu wa damu urafiki au ujirani. Pamoja na vigezo hivyo tabia njema ndio msingi mkuu wa utenzi wa mchumba.

Uchunguzi maalum wa tabia za wachumba kwa pande zote mbli hufanywa kabla ya kuwasilisha posa rasmi. Uchunguzi huu hufanywa na wazee wa upande husika ili kujiridhisha. Njia moja ya uchunguzi huo ni kupitia kwa majirani na watu wanaowaelewa wachumba hao. Mara nyengine mzee wa familia ya bwana harusi mtarajiwa huenda katika familia ya bi harusi mtarajiwa ili kuchunguza tabia zake. Ili kuweza kuonekana vizuri mtoto wa kike (mchumba) hutumwa maji ya kunywa kwa ajili ya mgeni au hutakiwa kumuandalia chakula mgeni. Lengo ni kutoa fursa kwa mzee na bwana harusi mtarajiwa wanaotaka kuposa kumuona mchumba vizuri tabia, sura na umbo lake kabla ya kuamua kuwasilisha posa rasmi. Na kwa upande wa bi harusi mtarajiwa baada ya wageni kuondoka huulizwa kama yule mwanamme aliyemuona anamtaka amuoe au laa.

Mara nyengine wachumba hupewa fursa ya kukaa kando kidogo ili wazungumze machache na kuweza kuelewana vizuri zaidi. Fursa hii huwa chini ya uangalizi wa wazee husika ili kuepusha kwenda kinyume na maadili. Bi Aisha Yazid Haji umri miaka 46 amenukuliwa akisema "mimi nilipoolewa mchumba wangu sikumjua wala sikuwa na maelewano naye bali ni wazee tu ndio walioamua niolewe na sikuweza kukataa". Kwa kawaida mwanamme au mwanamke akitaka kuoa au kuolewa kwa mara pili baada ya kuacha au kuachwa huwa huru kuchagua mchumba mwenyewe kwa ushauri wa wazee.

Hata hivyo kutokana na mabadiliko ya kijamii yanayotokana na athari za kigeni watoto (wachumba) hivi sasa hupenda kuwa huru kuchagua mke au mume anayempenda mwenyewe. Bali katika desturi za kizanzibari mtoto huwa hana maamuzi ya mwisho ya kuoa au kuolewa mbele ya mbele ya wazee wake. Mzazi ndiye mwenye maamuzi ya mwisho baada ya kuelewa tabia za mchumba mtarajiwa. Baada ya wazazi kuridhika na tabia za mkwe (mchumba wa mtoto wao) wazazi wawili baba na mama hukaa na kuamua, pindi wazazi wakikubaliana na mchumba huyo mshenga (mposaji au mjumbe) huteuliwa ili kuwasilisha posa nyumbani kwa wazazi wa mchumba wa kike mtarajiwa.

**2.3 POSA/KUCHUMBIA**

Ni kitendo cha kuwasilisha ombi la kupatia mchumba katika familia ya mwanamke. Upande unaowasilisha posa ni ule wa mwanamme (muoaji). Kitendo hiki hutekelezwa na mshenga (mposaji) ambaye huteuliwa na mzazi wa mtoto wa kiume au muoaji mchumba mwenyewe pindi ikiwa harusi ya mara ya pili.

**2.4 Mshenga**

Mshenga ni mjumbe ambaye huteuliwa na familia ya bwana harusi kwenda kuwasilisha posa katika familia ya bi harusi mtarajiwa. Sifa za mshenga ni yule mtu mwenye tabia nzuri, mwenye maarifa na heshima mbele ya jamii au aliye maarufu sana katika jamii husika. Mshanga lazima awe mwanamme baleghe mwenye akili timamu, muislamu na aliyewahi kuoa. Kwa kawaida posa (ombi) hukamilika kwa vipindi viwili kipindi cha kwanza ni kuwasilisha posa (ombi) nyumbani kwa bi harusi mtarajiwa. Baada ya kuwasilishwa posa wazazi wa bi harusi wa upande wa kuumeni na kukeni (baba na wajomba) hukutana na kuamua ama posa ikubaliwe au ikataliwe.

Kipindi cha pili ni cha kuchukua majibu ya posa kama imekubaliwa au imekataliwa. Siku maalum huteuliwa ya kutolewa jibu. Mshenga ndiye anayepaswa kwenda kuchukua jibu kutoka kwa wazee wa mwanamke. Pindi posa ikikubaliwa rasmi wazazi wa mtoto wa kike humpangia siku maalum mshenga (mjumbe) kwenda kutajiwa mahari wanayopaswa kulipa kwa ajili ya yule binti aliyeposwa.

**2.5 Mahari**

Mara nyingi mahari huwa fedha taslim au fedha na vitu Fulani kama kitanda, kabati, fanicha na kadhalika. Kima na aina ya mahari huamuiliwa na wazazi ingawa mtoto (wa kike) naye pia hutakiwa aoneshe ridhaa yake juu ya mahari iliyotajwa na wazazi wake. Mahari huwa ni mali ya mchumba anayeolewa kama ni zawadi ya kujitunza kwake, ridhaa pia ni mila inayotokana na imani ya dini ya kiislamu.

Katika mila za kijadi za wazanzibari mahari pia hujumuisha kiasi kidogo cha fedha kwa ajili ya mkaja wa bibi na kilemba cha babu. Hizi ni fedha wanazopewa babu na bibi waliomzaa bi harusi mtarajiwa. Hii ikiwa ni sehemu ya mila na utani kwa mjukuu wao. Fedha hizi huwa si sehemu ya mahari halisi.

Siku ya kuwasilishwa mahari huteuliwa rasmi. Wazazi wa bi harusi mtarajiwa wa kuumeni na kukeni hualikwa na mshenga naye husindikizwa na wazee wenzake hasa kutoka upande wa mama wa bwana harusi mtarajiwa ili kushuhudia kutolewa kwa mahari hayo. Tukio hili huambatana na tafrija ndogo ama ya chai, kahawa au juisi pamoja na vitafunio kama tende, halua, visheti, maandazi au mikate. Baada ya kuwasilisha mahari Mshenga hutakiwa ataje siku rasmi ya kufanyika kwa harusi yenyewe. Siku ya harusi hutolewa na wenye kuoa bali hata wanaoolewa nao kama wanapendekezo tofauti na maamuzi ya waposaji huzingatiwa na mara nyengine hukubaliwa. Katika kipindi chote hicho bi harusi na bwana harusi watarajiwa kimila na kidesturi hawatakiwi kukutana faragha kama wapenzi.

Baada ya mahari kutolewa familia ya bi harusi mtarajiwa hubeba jukumu la kumchunga na kufuatilia nyendo za mtoto wao kwa karibu zaidi kuliko ilivyokuwa hapo kabla ya kuposwa ili kujikinga na aibu inayoweza kutokea kabla ya harusi. Hivyo bi harusi hupangiwa muda wa kutoka na kurejea nyumbani, jinsi ya kuvaa nguo zake, watu wa kuambatana nao na pia hutakiwa kupunguza safari za mara kwa mara zisizo na umuhimu.

Bwana harusi mtarajiwa naye hutakiwa na wazee wake kuchunga tabia zake na kujiepusha na vitendo vyenye kwenda kinyume na maadili ya jamii. Bwana harusi mtarajiwa hutakiwa ajiepushe na kuchanganyika na wasichana wengine ovyo, ulevi, uhuni na tabia nyengine mbaya. Pindi upande mmoja kati ya pande mbili hizi ukipoteza imani juu ya tabia za mmoja kati ya wachumba watarajiwa posa hiyo huvunjika na harusi haitafanyika tena. Kama upande wa bi harusi ndio sababu ya kuvunjika kwa posa watalazimika kurejesha mahari iliyotolewa, na kama upande wa bwana harusi mtarajiwa ndio chanzo cha kuvunjika posa mahari iliyokwishatolewa hayatorejeshwa tena.

**2.6 Singo na Unyago**

Singo ni kitendo cha kimila ambacho hujumuisha kufanyiwa usafi wa mwili wa bibi harusi au bwana harusi mtarajiwa na kupewa mafunzo yanayohusiana na maisha ya ndoa. Singo hufanywa na wanawake watani wa bi harusi au bwana harusi. Miongoni mwa malengo makuu ya singo ni kusafisha miili ya maharusi kwa kuondosha nongo (udongo) mwilini, kuwanyowa sehemu zote za mwili na kungarisha ngozi ya ngozi zao ili zionekane tofauti na siku za kawaida na kuwa na mvuto kwa mwenzake (mchumba wake) na jamii kwa jumla. Singo pia husaidia kuondosha harufu mbaya mwilini na kufanya mwili unukie vizuri kwa kipindi chote cha uharusi.

Madawa maalumu yanayotokana na miti shamba hutumika kwa ajili ya kumsingia bibi au bwana harusi kama vile dalia, liwa, karafuu, maji ya mawardi, asumini kavu, tuwi la nazi, marashi mafuta ya nazi na kadhalika. Madawa haya husagwa na kuchanganywa pamoja na kuwekwa kwa siku kadhaa ili yaweze kuiva vizuri kabla ya kutumika. Vifaa vyengine muhimu vinavyotumika katika singo ni kama mehi, kinu, kata na chetezo. Bi harusi au bwana harusi husuguliwa mwili mzima kwa kutumia mchanganyiko wa madawa haya. Bi Jina Ali Ameir mkaazi wa Chumbuni alisema "katika harusi ya Kizanzibari bi harusi lazima asingwe kwa kutumia vimamo maalum kama liwa, mawardi, asumini na kadhalika. Bila ya kufanya ada hiyo harusi huwa na kasoro kubwa".

Washiriki wakuu wa singo la bi harusi au bwana harusi ni pamoja na madada, mabibi (watani au chevi) na wanawake wengine waalikwa lakini si watu ambao bi harusi au bwana harusi anapaswa kuwaheshimu. Msingwaji ndiye mshiriki mahsusi na muhimu sana siku hiyo. Matayarisho maalum hufanywa kama vile kuwaalika washiriki, kuaandaa vifaa vya singo na dhifa.

Mbali ya singo ambalo bwana harusi mtarajiwa hufanyiwa na watani wake mababu nao wa bwana harusi pia humpa mafunzo mjukuu wao. Mababu wa bwana harusi humfunza mjukuu wao tabia za ujasiri ukakamavu, uvumilivu, kutunza siri za mke kumtimizia mahitaji ya mkewe kwa kufanya kazi kwa bidii zaidi na kutunza mke vizuri kwa kumpatia mahitaji yake yote ya lazima.

Singo hufanyika katika maeneo ya faragha kutokana na maudhui ya nyimbo, uchezaji na mavazi ya washiriki ambayo huwa nusu uchi ili kumfunza bi harusi kwa mfano halisi kama uvaaji wa shanga, sauti ya kuzungumza na bwana, tabia za upole na heshima kwa mume, jinsi ya kucheza viuno wakati wa mapenzi nakadhalika. Kwa kawaida singo hufanywa chumbani au ukumbini ndani ya nyumba. Eneo ambalo hakuna watoto wala wanaume wanaopita pita. Milango na madirisha hufungwa ili sauti isitoke nje na kuwafikia wasiohusika.

Mara nyingi singo hufanyika wakati wa jioni baada ya sala ya laasiri au usiku baada ya sala ya magharabi. Na hudumu kwa muda wa masaa mawili (2) au zaidi. Huu ni wakati ambapo watu wote huwa wameshamaliza harakati zao za mchana kutwa na huweza kuhudhuria kikamilifu katika singo hilo. Ili kuondosha haya wakati wa singo baadhi ya wasingaji hunywa uji wa kungu manga ambao hupikwa makusudi kwa ajili hiyo. Ni uji unaopikwa kwa unga wa mahindi au mtama na kuchanganywa na kungu manga ya unga. Uji huu hupelekea mtu kupata nishai ya ulevi na kutokwa na haya kwa mambo anayoyafanya mbele ya wenzake.

Wakati kazi ya usingaji ikiendelea washiriki hutumia vitumbuizo mbali mbali kama vile nyimbo, majigambo, makofi, kucheza (kukata viuno), kuigiza namna ya tendo la ndoa (kujamiiana) linavyofanyika yote hayo yakiongozwa na mlio wa ngoma aina ya msondo au makofi yenye kupigwa kwa mpangilio maalum. Ni tukio linaloambatana pia na vifijo vigelegele na vicheko vya furaha na dhihaka.

**2.7 Unyago**

Mara nyengine singo hufanywa kwa kutumia unyago. Ni ngoma ya kijadi ya kumfunza bi harusi maisha ya ndoa tabia za mke mwema, njia ya kutunza na kuimarisha mapenzi kwa mume na familia yake, malezi na tabia njema. Singo na unyago hunogeshwa na nyimbo mbali mbali ambazo kwa kawaida huwa ni za matusi na mafumbo. Nyimbo hizi huwa haziimbwi hadharani wala katika eneo lenye watu wanaoheshimiana. Bibi Mwanajuma Ali Khamis mkaazi wa Muungano mwenye umri wa miaka 51 alitoa mifano ya nyimbo hizo kama vile:-

1. "Bismillahi ndiyo ya kwanza ya kuanzia, Hiyo ni ila kwa mwanamke kutwa kiguu na njia, Mume anakwao atakukimbia.

Nyimbo inamfunza bi harusi kuwa na tabia ya kuanza na bismilahi kwa kila atakachokifanya ili maisha yake yawe na heri na baraka. Pia inamfunza bi harusi tabia ya kukaa (kutulia) nyumbani kwa mumewe na kuacha kutangatanga ovyo kwani si tabia nzuri ya mwanamke aliyeolewa. Halkadhalika nyimbo hii inaonya pindipo mke akienda kinyume na mafundisho hayo ataachwa na mumewe.

2. "Usilie usilie wee! Mtoto, oyaa! Ukaniliza na miye wee! Mwana, oya we! Mwana, oya wee! Mtoto nyamara kulia, ukaniliza na miye Machozi yako yaweke we mtoto, Nikifa unililiye we mtoto."

Nyimbo hii inamfunza bi harusi kuwa mvumilivu na mstahamilivu wa shida na mitihani mbali mbali itakayomkabili katika kipindi baada ya kuolewa akianza maisha ya familia yake. Lengo ni kumpa moyo na ujasiri katika maisha ambayo hajayazowea hasa kuwa mbali na wazee, ndugu na jamaa zake.

3. "Kanga wee, kanga wee! Kanga kupekuwa kanga ndiyo kazi yake".

Maana ya nyimbo hii ni kwamba kanga ni ndege mwenye tabia ya kupekuwa kwa miguu yake ili apata chakula chake. Pia kanga ni nguo ambayo huvaliwa zaidi na wanawake na ni moja ya vazi mashuhuri kwa bi harusi wa kizanzibari (kisutu). Hivyo nyimbo inamfunza bi harusi kwamba baada kuolewa mume atakuwa na haki ya kumpapasa na kumgusagusa mkewe wakati wowote kwani hiyo ndiyo tabia ya mume na si ila bali ni mapenzi. Aidha ni kumfunza bi harusi kuwa tayari kumpa haki (mapenzi) yake mumewe ambayo ndiyo msingi wa ndoa yao. Bi Mwajuma alisisitiza kwamba kitendo cha kutompa mapenzi mume ni aibu kwa mtoto (bi harusi) na wazazi wake. Hivyo lazima bi harusi afunzwe vizuri kabla ya kuolewa".

1. "Mronge huo, mronge huo! Mronge kunyorora nyorora, mronge ndio mboga".

Mronge ni aina ya mboga ya majani ambayo baada ya kupikwa huwa laini na yenye kuteleza. Nyimbo hii inamfunza bi harusi ambaye ndiyo mara ya kwanza kuolewa kwamba wakati atakapofanya mapenzi na mumewe baada ya kuolewa ataona mtelezo katika sehemu za siri hiyo ndio tabia ya mapenzi hivyo asiogopa au kushangaa. Aidha inamuonya asiwe na haraka wakati anapofanya mapenzi na mumewe.

Baada ya kusingwa bi harusi hupelekwa chooni kwa ajili kukogeshwa. Dhifa maalumu huandaliwa wakati wa singo kwa ajili ya wasingaji na bi harusi au bwana harusi. Dhifa hii huwa chai, mikate na mchuzi wa kuku au nyama ya ngombe. Kwa kawaida dhifa hutolewa baada ya kumalizika singo. Vile vile washiriki wanaohudhuria singo huchukua zawadi mbli mbali kwa ajili ya msingwaji kama vile kanga, vitambaa, vyombo vya nyumbani, manukato, mapambo nakadhalika.

**2.8 KUPAKA HINA**



**Biharusi anapakwa hina**

Hina ni unga wa rangi ya kijani iliyokoza unaotokana na mmea maarufu mhina. Ni moja kati ya vipengele muhimu sana katika ustaarabu wa mswahili hususan katika mapambo. Hina huchanganywa na maji kidogo na kuwa kama uji mzito. Pia hutiwa maji ya ndimu ili kuongeza ukali wa hina hiyo. Mchanganyo huu huifanya hina kuwa nyeusi. Hina hutumiwa kumpamba bi harusi lakini pia wenyeji wa visiwa vya Zanzibar huitumia sana katika siku zao za furaha kama sikukuu, harusi, sherehe za siku ya kuzaliwa nakadhalika.

Kwa kawaida katika harusi za kizanzibari bi harusi hupakwa hina siku chache kabla ya kuolewa rasmi. Kimila bi harusi wa kizanzibari huwa hapakwi hina nyumbani kwao kwa wazazi wake. Somo wa bi harusi ndiye mwenye jukumu la kumpaka hina bi harusi ambaye naye anaweza kuwatafuta watu maalumu wenye ujuzi na uzoefu sanaa ya upakaji hina. Hina hutayarishwa siku mbili au zaidi kabla ya kuanza kutumika ili hina iwe nzuri na yenye kukoza.

Hina ya bi harusi hutofautiana kidogo na hina za watu wa kawaida hina ya bi harusi hukoza (huwa nyeusi sana) na hupakwa sehemu kubwa zaidi ya mwili wake. Katika hatua za mwanzo za upakaji wa hina, hina huonekana katika rangi nyekundu bali kadiri upakaji unapoendelea hina hiyo hukoza na kuwa rangi nyeusi iliyokoza. Hina ya bi harusi hupakwa kwa muda usiopungua siku tatu kwa kupaka na kufuta hadi ikoze na iwe nyeusi.

Katika utamaduni wa kizanzibari upakaji hina hususan hina ya harusi huwa ni jambo lenye kuhitaji stara. Upakaji wa hina ya bi harusi mara nyingi hufanyika ndani ya nyumba, ukumbini, uwani au katika chumba kisichotumika. Eneo la faragha lililojitenga na macho macho ya watu ndio linalotumika zaidi kwa kazi hii. Kitendo cha kumuepushia bi harusi na macho ya watu wakati wa kupakwa hina ni cha kimaadili katika jamii ya wazanzibari. Kutumia maeneo maalumu husaidia kustiri mwili wa bi harusi ili usionekane na watu wasiopaswa. Wakati biharusi anapopakwa hina sehemu kubwa ya mwili wake huwa wazi ili kuruhusu hina ikauke vizuri katika maeneo yote. Bali hata maadili ya kizanzibari hayaruhusu mwili wa mwanamke kuonekana na mwanamme hasa anaefaa kumuoa. Pia husaidia kuepusha baadhi ya wanaume kumtamani bi harusi kutokana na kupendeza kwake kwa hina aliyopakwa.

Hina hukaushwa kwa kutumia moto mwepesi ambao mara nyingi huwa wa makumbi au mwanga wa jua. Lengo kuu la upakaji wa hina kwa bi harusi ni kumpamba ili apendeze zaidi kuliko siku za kawaida. Hina huongeza mvuto kwa bi harusi mbele ya mumewe. Bibi Sharifa Mwinyi mkaazi wa Misufini mwenye umri wa miaka 49 alisema "Hina ni urimbo unaweza kumnasa mwanamme akatulia ndani kwa mkewe hata nje asitamani. Aliendelea kufafanua kwamba hina humbadilisha mwanamke na kuwa mpya kama nguo iliyotoka boksini sasa hivi. Maelezo haya kutoka kwa bi Sharifa yanaonyesha nafasi ya hina katika mapambo ya biharusi wa kizanzibari.

**2.9 Kupambwa Bi harusi na Bwana harusi**

Hili ni tukio muhimu sana kwa maharusi wa kizanzibari kwani harusi ni sikukuu kubwa ya wazanzibari. Maharusi hupambwa siku ile ya kuoana (akdi). Watu maalumu hutumika kuwapamba maharusi kwa kutumia vifaa mbali mbali vya kupambia. Mambo haya huonekana katika mavazi, mapambo ya mwilini, nywele, na hata vitu vya ziada ambavyo huchukuliwa au kushikwa na bi harusi au bwana harusi..

Kwa upande wa mavazi, mavazi maalumu huvishwa bi harusi siku ya harusi. Kwa bi harusi wa kizanzibari vazi rasmi la asili ni kanga za kisutu.



**Bi harusi na mapambo yake**

Nywele nazo hutengenezwa vizuri kwa kuchanwa kwa kutumia mafuta ya nazi yaliyoungwa vizuri kwa viungo mbali mbali na kufanya yanukie vizuri. Bi harusi wa kizanzibari husukwa msuko maalumu aina ya mnyoosho au shikamoo bibi.

Na bwana harusi naye siku hiyo hupambwa vizuri kwa kutumia mavazi ya kitamaduni. Mavazi ya bwana harusi wa kizanzibari huwa kanzu ya msikitini nyeupe, koti, joho, kofia ya kiua, kilemba, mkashda na viatu vya sandali (hususan) kubadhi. Wasfu wa bwana harusi wa kizanzibari huaksi sana utamaduni na mila za mswahili zinazotokana na maingiliano makubwa ya damu na tabia kati ya watu wa mwambao wa frika mashariki na bara arabu. Baadhi ya mabwana harusi wa kizanzibari pia hushika fimbo mkononi hasa wanapovaa vazi la joho na kilemba siku hiyo ya harusi. Wengine katika vazi hilo hilo hufunga jambia kiunoni ikionesha utamaduni Kanga za bi harusi huwa mbili moja hujifunga kifuani na nyengine hujitanda kutoka kichwani na kuteremka mabegani. Hata hivyo katika siku za karibuni uvaaji huu umebadilika kidogo kwani baadhi ya ma harusi hivishwa kanzu ndefu inayoshuka hadi chini ya magoti na hufunikwa kanga mpya aina ya kisutu au

mtandio kutoka kichwani na kushuka mabegani akibakishwa sehemu ndogo ya paji lake la uso.

ISSN 3104-6371



**Biharusi na kanga ya kisutu**

Mapambo ya mwilini kwa bi harusi ni kama bangili, kidani, pete, poda, wanja, rangi ya mdomo, pamoja na hina ambayo hupakwa tokea kabla ya siku ya harusi rasmi.

wa warabu wa Omani ambao kwa muda mrefu walitawala Zanzibar tokea mwanzoni mwa karne ya 19. Bwana harusi pia siku hiyo hutengenezwa nywele zake vizuri kwa kupunguzwa na kuwa ndogo na safi.

Bwana harusi na mavazi yake

Katika kipindi hiki cha kupambwa maharusi, kiutamaduni hawatakiwi kuonekana onekana na watu wasiohusika. Hivyo mwanamke (bi harusi) huwekwa katika nyumba maalum ambapo harusi hiyo itaolewa. Akiwa ndani bi harusi watu maalum (watani wake) humuhudumia kwa kumpamba, kumpangusa jasho, kumuweka sawa nguo yake, kumzungumzisha, kumliwa, za kumpa chakula na hata kumpeleka msalani (chooni) akihitaji.

Siku hiyo bi harusi huwa kama malkia katika kiti chake cha enzi.

Bwana harusi naye wakati wa kupambwa na baada ya kupambwa hufichwa katika nyumba isiyofahamika na kila mtu. Hubakia katika eneo hilo hadi muda mfupi kabla ya bwana harusi, wapambe na msafara wake kuelekea katika eneo la harusi (Akdi).

**2.10 Kupima Nyumba Kuangalia Siku**

Katika mila za jadi siku na wakati wa kufanyika harusi (Akdi) lazina ichunguzwe na ithibitishwe kwa makini. Hii ni kutokana na imani kwamba si kila siku huwa njema baadhi ya siku huwa na nuhusi na mikosi ambayo inaweza kuwapata maharusi au familia zao pindi harusi ikifanywa siku kama hizo. Wazazi wa bwana harusi ndio hasa wenye kuangalia na kutoa siku na saa ya harusi. Kuangalia siku ya kufanyika kwa harusi hufanywa kwa utaalamu maalum na waganga wa jadi. Waganga hao hutumia taaluma yao ya uganga kuagua au kubashiri ni siku gani itakuwa njema na salama kwa kufanya harusi. Kutokana na imani ya waswahili wa kizanzibari iliyojengeka katika misingi ya kidini, wanaamini kwamba siku ya ijumaa hua ni siku njema isiyo na aina yoyote yamikosi wala nuhusi. Hivyo kwa imani hiyo harusi nyingi za kizanzibari hufanyika siku ya Ijumaa hasa baada ya sala ya ijumaa au laasiri.

**HITIMISHO**

**4.1 Hitimisho**

Kutokana na utafiti wa harusi za kizanzibari umebainisha kwamba harusi huwa na sehemu mbili kuu matayarisho (hatua za awali) na Akdi (Kufungisha Ndoa)

**1.4 الخلاصة**

من خلال البحث الذي أُجري حول حفلات الزفاف في زنجبار، تبيّن أن حفل الزفاف يتألف من جزأين رئيسيين: التحضيرات (الخطوات التمهيدية) و"العقد" (تكريس الزواج).

**MAREJEO**

1. Jesper Kirknaes, 2005 Zanzibar Heritage Copenhagen, Denmark

2. Makumbusho ya Taifa Zanzibar (Beit el Ajaib)

3- التراث الثقافي التنزاني في كتاب «رحلة إلى مهد البشرية

4- عرس الزين_ للكاتب الطيب صالح